

02.04.2026

TANGAZO LA ZABUNI YA MACHAPISHO YA VITABU/HATI KWA MATUMIZI YA OFISI
MSIMU 2026/2027

Zabuni na: KCU/G/2026/2027/02

1. KCU (1990) LTD imetenga fedha kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kimkataba na mtoa huduma ya Uchapishaji vitabu/hati kwa msimu 2026/2027
2. Kampuni/Mtu binafsi anayotambulika anakaribishwa kuleta maombi ya zabuni hii ili kutoa huduma ya Uchapishaji vitabu/hati.
3. Mwombaji aambatishe nakala ya leseni ya biashara TIN pamoja na VRN.
4. Mwombaji aambatishe nakala ya usajili wa kampuni
5. Mwombaji aambatishe nakala zinaoonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya.
6. Ombi la zabuni liwe na jina, anwani halisi la mwombaji na mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
7. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**
8. Mwombaji afike katika ofisi ya manunuzi kwa ajili ya kupewa orodha ya vitabu vitakavyochapishwa kwa msimu 2026/2027.
9. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 3-8 vilivyo tajwa hapo juu.
10. Bahasha ya maombi ifungwe vizuri kwa lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI YA ZABUNI YA MACHAPISHO YA VITABU/HATI KWA MATUMIZI YA OFISI MSIMU 2026/2027"** kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.

11. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
12. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

